DOKEZO LA HISTORIA:

# Jinsi ya kuwasaidia manusra wa unyanyasaji wa kijinsia wakati mtetezi wa GBV hayupo kwenye eneo lako:

## Kijitabu cha Mwongozo wa hatua kwa hatua kwa watendaji wa kibinadamu Toleo la 2.0

Mnamo Septemba 2015, Miongozo ya Kuunganisha Mbinu za kupambana na Unyanyasaji wa Kijinsia katika Mazingira ya Kibinadamu ya IASC (Miongozo ya GBV) ilizinduliwa. Katika muda wa 2016 na 2017, Timu ya Msaada wa Utekelezaji wa Miongozo ya GBV iliwafundisha watendaji wa kibinadamu zaidi ya 2,500 katika sekta 11 na nchi 18 kuhusu jinsi ya kupunguza hatari zinazohusiana na unyanyasaji wa kijinsia katika mipango yao.

Katika mazingira tofautitofauti na sekta, kuwafundisha washiriki kuonyesha mapendeleo yao na hitaji la muhtasari, jinsi ya kutafuta raslimali kuhusu ***jinsi ya kumsaidia manusra kutokana na unyanyasaji wa kijinsia (GBV) wakati hakuna mtetezi wa GBV (kwa kujumuisha njia ya rufaa au mtaalamu wa GBV/kituo cha masuluhisho) katika eneo lao.*** Baada ya mashauriano na watendaji wengine na mbinu za uratibu, ni dhahiri kwamba changamoto hii hujitokeza tena katika mazingira tofautitofauti na katika watetezi wa aina nyingi.

Ili kujaza pengo hili, Kikundi cha Kufanyia kazi Pamoja kilichoundwa na Kikundi cha Urejeleo wa Miongozo ya GBV na Eneo la Uwajibikaji wa GBV kiliunda kifurushi cha raslimali kuhusu jinsi ya kumsaidia manusra kutokana na GBV wakati hakuna njia ya rufaa ya GBV au kituo cha masuluhisha ya GBV ("Kijitabu cha Mwongozo"), kama kiongozaji cha pamoja cha Miongozo ya GBV. Kifurushi hiki cha raslimali kiliundwa kwa kutumia wataalamu kutoka kwa wanachama wa Kikundi cha Kufanya kazi, wahakiki wan je na washiriki wa mashauriano kuanzia Septemba 2017 hadi Februari 2018; Zaidi ya hayo, raslimali inawiana na zana zilizopo za kilimwengu kama vile Rafiki Dhabiti wa Nguzo ya Makazi ya GBV (Shelter Cluster's GBV Constant Companion) na Miongozo ya IRC/UNICEF ya Kutunza Watoto Walionusurika kutokana na Unyanyasaji wa Kingono.

**Toleo la Februari 2018 la kifurushi cha raslimali ya Kijitabu cha Mwongozo** linajumuisha matoleo yaliyochapishwa, ya mtandaoni na ya programu ya simu katika Kiarabu, Kiingereza, Kifaranza na Kihispania.

## Kuhusu Miongozo ya GBV

Miongozo ya GBV ya 2015 (ilihakikiwa kutoka kwenye toleo la 2005) ni zana ya kufanya kazi, iliyojaribiwa ambayo inatoa mwongozo kwa watetezi wa kibinadamu na jamii zilizoathirika kwa migogoro na majanga ya kiasili kwenye hatua muhimu za kupambana na hatari zinazohusiana na unyanyasaji wa kijinsia (GBV)-na kusababisha mipango salama na yenye ufanisi zaidi. Miongozo ya GBV ni ya watu wasiokuwa wataalamu wa GBV, ambao wanaweza na wanafaa kuchukuwa hatua katika shughuli za kila siku za sekta zao wenyewe ili kupunguza hatari zinazohusiana na GBV. Mkakati wa Utekelezaji wa miaka mitatu sasa unaanzishwa ili kuongeza viwango vya mapendeleo, uhamasisho na matumizi ya Miongozo ya GBV.
Kwa maelezo Zaidi, tembelea www.gbvguidelines.org.

### JE, LENGO LA KIFURUSHI CHA RASLIMALI YA KIJITABU CHA MWONGOZO NI NINI?

Lengo la kifurushi hiki cha raslimali ni kutoa maelezo dhabiti kwa watendaji wote wa kibinadamu kwa namna ya kiongozaji rahisi cha kufuata na cha kubeba:

→ Jinsi ya kumsaidia manusra kutokana na unyanyasaji wa kijinsia aliyejifunua kwako mahali ambapo ***hakuna mtetezi wa unyanyasaji wa kijinsia*** *(kwa kujumuisha njia ya rufaa au kituo cha masuluhisho ya GBV)* ***anayepatikana katika eneo lako.***

Kifurushi cha raslimali kinatuma viwango vya kilimwengu katika kutoa msaada wa msingi na maelezo kwa walionusurika kutokana na GBV bila kufanya madhara zaidi. Tunahimiza utumiaji wa raslimali hii katika mazingira yako kwa msaada wa mtaalamu wa GBV.

### JE, NI KITU GANI KIMEJUMUISHWA KATIKA KIFURUSHI CHA RASLIMALI YA KIJITABU CHA MWONGOZO?

1. **Dokezo hili la Historia** ni la kutambulisha raslimali na kutoa ujumbe muhimu kwa ajili ya utetezi na uratibu.
2. **Karatasi ya Vidokezo vya Mtumiaji,** inalenga wasimamizi wa mpango, waratibu wa kiufundi, viongozi wa timu na watendaji wengine kama hao katika sekta zote ili kusaidia katika kutaarifu na kuhimiza timu zao kutumia Kijitabu cha Mwongozo na kumsaidia manusra kutokana na unyanyasaji wa kijinsia katika tukio kwamba manusra

*(over)*

anajifunua kwako au kutafuta msaada wao.

3. **Kijitabu cha Mwongozo**, kinalenga watoaji wa mstari wa mbele katika nguzo/sekta zote, kukitumia kama urejeleo rahisi kuhusu jinsi ya kumsaidia manusra kutokana na unyanyasaji wa kijinsia ikiwa manusra anaomba msaada wao katika mazingira ambayo hakuna mtetezi wa GBV/njia ya rufaa inayopatikana katika eneo.

### JE, NI NANI ANAYEWEZA KUTUMIA KIJITABU CHA MWONGOZO?

Kijitabu cha Mwongozo kinalenga watu wasiokuwa wataalamu wa GBV walio kwenye mstari wa mbele wa kutoa huduma kwa jamii zilizoathirika, kwa kujumuisha wahamasishaji wa usafi, wafanyakazi wa afya katika jamii, wasimamizi wa kambi, vitovu vya masuluhisho ya kiusalama n.k.

### JE, NI KITU GANI KIMEJUMUISHWA KATIKA KIJITABU CHA MWONGOZO?

Kijitabu cha Mwongozo kimeundwa kuwa raslimali ya kufanyia kazi wakati manusra anafunua tukio lao kwa mtendaji yeyote wa kibinadamu. Kinajumuisha chati rahisi ya kusoma, urejeleo wa haraka wa mambo ya Kutendwa na Yasiyofaa Kutendwa, na ufikiaji haraka kwenye orodha ya matukio yah atua kwa hatua zinazofuata mpangilio ulioandaliwa, wa kuangaliwa, kusikizwa na kuunganishwa.

Kijitabu cha Mwongozo kinajumuisha mazingatio ya Watoto na vijana, walio wachache kingono na kijinsia/LGBTQI, manusra walemavu na manusra wanaume.

### JE, NI WAPO NINAPOWEZA KUKIPATA?

- Mtandaoni kwenye www.gbvguidelines.org and www.gbvaor.net katika matoleo ya mwonekano wa juu na chini ya kuchapishwa.
- Pakua kwenye Google Play au duka la iTunes. Tafutiza "Kijitabu cha Mwongozo cha GBV."

## Ujumbe muhimu wa utetezi na uratibu

1. Kujumuisha hatua za kupambana na hatari za GBV, kama zile zilizo kwenye Miongozo ya IASC GBV, si tu jukumu muhimu la watendaji wote wa kibinadamu, pia huboresha ufanisi wa mwitikio wa kibinadamu katika sekta zote.
   a. Kulingana na kanuni ya "Usidhuru" na tamko la Ulinzi wa Umuhimu wa IASC, watetezi wa kibinadamu katika sekta zote wana jukumu la kuunda na kutekeleza mipango yao kwa njia inayopunguza hatari za GBV na kuhakikisha ufikiaji kwa vikundi dhaifu.
   b. Wakati mipango ni salama na kufikiwa Zaidi, watu wengi hunufaika, na matokeo kijumla huboreka; kwa upande mwingine, kukosa kushughulikia masuala ya GBV kunadhoofisha ufanisi wa mbinu za kibinadamu katika sekta zote. .
2. **Ukosaji wa usawa wa kijinsia ulioko huwafanya wanawake na wasichana hasa kuwa dhaifu katika mgogoro wa namna hii, na kuongeza hatari yao kwa namna nyingi ya GBV,** kwa kujumuisha unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa kinyumbani, ndoa ya lazima na utumiwaji vibaya wa kingono na udhalimu.
   a. Wakati familia zinashindwa kutimiza mahitaji yao ya kimsingi, wanawake na wasichana wanalazimika kutumia mbinu hatari za kukabiliana na kuongeza hatari yao kwenye GBV.
   b. Wakati wanawake na wasichana wamekosa nafasi za kazi za ushiriki wa maana, mahitaji yao na ufikiaji huduma mara nyingi hauonekani katika utoaji wa msaada wa kibinadamu.

**KUANGALIA MBELE:** Kikundi cha Kufanya Kazi kinachunguza jinsi ya kutoa raslimali zaidi katika hali ambazo kuna huduma tamba, huduma ambazo zinahitaji usafirishaji kwa huduma, au huduma za mbali kama namba ya simu ya moja kwa moja au gumzo la siri la mtandaoni. Wataalamu wa GBV pia wanachunguza modeli mpya za utoaji huduma ili kushughulikia, kuzuia na kukabiliana na GBV. Kikundi cha kufanya kazi pamoja kinatafuta kujenga zana na raslimali ili kutimiza mahitaji haya.

**PATA KUJUMUIKA:** Ikiwa ungependa kutumia Kijitabu cha Mwongozo katika eneo lako au kujumuika zaidi katika ukabilianaji na hatari ya GBV katika mazungumzo ya dharura, tuma barua pepe kwa gbv.guidelines@gmail.com.

**KUKIRI:** Working Group ingependa kutambua msaada mkuu wa kiufundi na wa uratibu wa wahakiki wa nje na washiriki wa mashauriano waliohusika katika kuandika kifurushi hiki cha raslimali kwa kujumuisha ACF, Uratibu wa Kambi na Nguzo ya Usimamizi wa Kambi, Eneo la Jukumu la Ulinzi wa Mtoto, Kikundi cha Kufanya kazi kati ya Mashirika kuhusu Afya ya Uzalishaji katika Mgogoro, Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu, IRC, Muungano wa Kiayalandi kuhusu Unyanyasaji wa Kijinsia, IOM, Shule ya London ya Usafi na Dawa ya Kitropiki, OXFAM, Shelter Cluster, Trócaire, UNFPA katika Kanda Yote ya Syria, UNHCR, UNICEF Sudan Kusini, WASH Cluster, World Vision South Sudan, WFP Sudan Kusini, Tume ya Wakimbizi ya Wanawake.